

**CONFIDENTIAL**  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA

Simu: Na. (255) 22 2116328 - 29  
Nukushi:(255 - 22)- 2118253  
Barua Pepe: information@tic.go.tz  
Tovuti:www.tic.go.tz  
Unapojibu Tafadhali taja:



Kiwanja Na. 9A & B  
Mtaa wa Shabaan Robert  
Sanduku la Barua 938  
11410 - DAR ES SALAAM

Kumb Na: **TIC/PP.10/042693/18**

**20 Oktoba, 2020**

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,  
Mkoa wa Tanga,  
S.L.P 5058,  
**TANGA**

**YAH: MALALAMIKO YA FIDIA YA MASHAMBA YA WANANCHI WA KATA  
YA MTIMBWANI NA KWALE WILAYA YA M KINGA**

Tafadhali rejea barua yako ya tarehe 26/08/2020 yenye Kumb.Na.LD/TA/GF/035/11 kuhusiana na mada tajwa hapo juu.

2. Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kinakiri kupokea barua yako tajwa hapo juu kuhusiana na madai ya fidia ya TZS 347,150,012.63 ya mashamba ya wananchi takribani 142 wa Kata ya Mtimbwani na Kwale Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga ili kupisha uwekezaji uliokusudiwa kufanywa na mwekezaji M/S Hengya Cement (TZ) Limited.
3. Kituo kinapenda kukufahamisha kuwa eneo husika bado halijamilikishwa kwa TIC na mwekezaji M/S Hengya Cement (TZ) Limited kupewa hati ya upangaji ya uwekezaji (Derivative Right) kutokana na kutokukamilika kwa hatua za awali za upatikanaji ardhi hii ikiwemo suala la fidia.
4. Zoezi la uhakiki wa madai ya fidia ya wananchi 142 wa Kata ya Mtimbwani na Kwale Wilaya ya Mkinga linaendelea kuratibiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga na kusimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.
5. Hivyo kupitia barua hii tungependa kukushauri kuwa uwasiliane na ofisi tajwa hapo juu kwa ajili ya kujua hatma ya madai ya fidia ya wananchi wa Kata za Mtimbwani na Kwale Wilaya ya Mkinga.

Tunatanguliza shukrani zetu.

  
R.A.Rasheli

**Kny: MKURUGENZI MTENDAJI**

**Nakala:** Katibu Mkuu,  
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
S.L.P 2908,  
**40477 DODOMA**

Kamishna wa Ardhi,  
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
S.L.P 2908,  
**40477 DODOMA**

Katibu wa Waziri,  
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
S.L.P 2908,  
**40477 DODOMA**

Katibu wa Mkuu wa Mkoa,  
Mkuu wa Mkoa wa Tanga,  
S.L.P 5095,  
**TANGA.**

Katibu Tawala (M),  
S.L.P 5095,  
**TANGA**

Katibu Tawala (W),  
S.L.P 2008,  
**MKINGA**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga,  
S.L.P 6005,  
**MKINGA**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Hengya Cement (Tz) Limited,  
S.L.P 600,  
**TANGA**